JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



IDARA YA UTAFITI NA UDHIBITI

MIANYA YA RUSHWA KATIKA UKUSANYAJI WA MAPATO KATIKA MAENEO YA KIMKAKATI

UCHUNGUZI KIFANI WA USAFIRI WA UMMA JIJINI DAR ES SALAAM

JANUARI, 2019

1.0 Utangulizi

Utoaji wa huduma bora za jamii ni jukumu la msingi la Serikali zote duniani. Kodi ndio chanzo muhimu cha mapato kinachoziwezesha Serikali kutoa huduma bora za kijamii. Kwa kulitambua hilo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imechukua hatua za makusudi za kuanzisha miradi mikubwa ya kutoa huduma za usafiri na maegesho katika jiji la Dar-es-Salaam. Miradi hiyo ni mabasi yaendayo kasi, Treni inayotoa huduma jijini, kituo cha mabasi Ubungo na maeneo ya maegesho ya magari.

Lengo kuu la kuanzisha miradi hii ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma za uhakika wakati wa kwenda na kurudi toka kwenye shughuli zao za uzalishaji za kila siku. Ili kuhakikisha miradi hiyo inajiendesha yenyewe na inakuwa endelevu, wananchi hutakiwa kuchangia huduma hizo. Lengo la utaratibu huu ni kuiwezesha Serikali kumudu gharama za uendeshaji/utawala kama vile mishahara ya watumishi pamoja na kugharamia matengenezo ya miundombinu yake. Hata hivyo, mapato yanayotokana na miradi hiyo yasiposimamiwa vizuri kwa sababu ya rushwa, si tu kwamba miradi hiyo itashindwa kujiendesha yenyewe, lakini pia azma ya Serikali ya kuwaletea maendeleo wananchi wake haitafanikiwa.

Katika siku za hivi karibuni kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali wa sekta ya usafiri, watunga sera na wananchi kwa ujumla kuwa usimamizi wa miradi hiyo hauridhishi na matokeo yake kusababisha Serikali kukusanya mapato chini ya kiwango kinyume na matarajio. Ni kutokana na sababu hizo, TAKUKURU ilionelea ni vema ikafanya utafiti kubaini endapo kuna mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo ya kimkakati na kisha kutoa mapendekezo au kuishauri Serikali namna bora ya kuiziba mianya yote itakayokuwa imebainika.

1.2 Maelezo ya Tatizo

Usafiri wa umma ni kichocheo muhimu cha kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Huduma za usafiri katika miji mikubwa unawawezesha watu kufika kwenye maeneo yao ya kazi kwa wakati, kufanya biashara zao kwa ufanisi, kuyafikia masoko bila kikwazo, husaidia matumizi bora ya rasilimali muda na kurahisisha mawasiliano. Ni dhahiri kuwa endapo muda mwingi utapotea njiani wakati wa kusafiri kutoka eneo mmoja kwenda lingine, shughuli nyingi za uzalishaji zitakwama na hivyo kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika nchi zinazoendelea kama Tanzania. Kwa

kuwa taarifa zilizopo ni finyu na kwa kutambua kuwa hata zile chache zilizopo hazielezi kwa kina tatizo la linalosababisha Serikali kukusanya mapato kinyume na matarajio yake, utafiti huu utajikita zaidi katika kuchunguza endapo kuna mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya kimkakati na kisha kupendekeza hatua stahiki zitakazoisaidia Serikali kuziba mianya ya rushwa itakayokuwa imebainishwa na utafiti.

1.3 Lengo kuu

Lengo kuu katika utafiti huu ni kubaini endapo kuna vitendo vya rushwa katika ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya kimkakati jijini Dar es Salaam.

1.4 Malengo mahususi.

Malengo mahsusi ya utafiti huu ni:

i. Kutathmini usimamizi wa sheria, kanuni na taratibu na miongozo katika ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo ya kimkakati
ii. Kubaini endapo matumizi ya mifumo ya kielektroni yamesaidia katika ukusanyaji wa mapato
iii. Kubaini endapo kuna mianya ya rushwa katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato na kupendekeza hatua zitakazoisaidia Serikali kuziba mianya ya rushwa itakayobainika.

1.5 Eneo, muda na idadi ya sampuli

Utafiti huu ulifanyika jijini Dar es Salaam ukihusisha miradi ifuatayo: Treni inayotoa huduma ya usafiri jijini, Kituo cha Mabasi cha Ubungo na Maegesho ya Magari. Sababu ya kuchagua eneo la Dar es Salaam ni kwamba miradi yote hii inatekelezwa katika jiji la Dar es Salaam na kwamba taarifa zote muhimu ambazo zingeweza kusaidia kujibu maswali ya utafiti huu zilikuwa zinapatikana katika mkoa huo. Aidha, utafiti huu umefanyika katika kipindi cha kuanzia mwezi Oktoba hadi Disemba 2018. Idadi ya sampuli iliyotumika katika utafiti huu ni 14.

1.6 Njia zilizotumika kukusanya taarifa

Ukusanyaji wa taarifa ulifanyika kwa kutumia njia kuu mbili:

i. Taarifa za Msingi (primary data) zilikusanywa kwa njia ya madodoso, *observation na* mahojiano ya ana kwa ana na Watendaji Wakuu wanaosimamia miradi hiyo
ii. Taarifa za Upili (Secondary data) zilikusanywa kwa kupitia mapitio ya nyaraka mbalimbali zinazohusiana na uendeshaji na utekelezaji wa miradi husika
iii. Kutembelea maeneo ya utafiti na kuona kiuhalisia namna ukusanyaji wa mapato unavyofanyika (observations).

4.0 Matokeo ya Utafiti

Sura hii inahusu uwasilishaji wa matokeo ya utafiti kutokana na taarifa zilizokusanywa uwandani. Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kubaini endapo kuna vitendo vya rushwa katika ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya kimkakati katika jiji la Dar es Salaam. Ili kufikia lengo hili, utafiti uliongozwa na madhumuni mahsusi (specific objectives) manne ambayo ni: (i) kubaini endapo kuna usimamizi duni wa sheria, kanuni na taratibu na miongozo katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kwenye miradi ya usafirishaji (ii) kubaini endapo matumizi ya mifumo ya kielektroni yamesaidia kuongeza mapato ya Serikali na (iii) kubaini endapo kuna mianya ya rushwa katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato na kupendekeza hatua stahiki zitakazoisaidia Serikali kuziba mianya ya rushwa iliyobainishwa na utafiti. Matokeo ya utafiti huu yatawasilishwa kufuatana na mpangilio wa madhumuni mahsusi kama inavyoonekana hapa chini.

4.1 Usimamizi wa Sheria, Kanuni, Taratibu katika Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato

Utafiti ulitaka kujua endapo ukusanyaji wa mapato unazingatia na kusimamia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Katika kulijibu swali hili asilimia 99.9% ya wahojiwa walikubali kwamba Mamlaka zinazosimamia utoaji wa huduma ya usafiri jijini zinaongozwa na sheria, kanuni, taratibu na miongozo; isipokuwa asilimia 0.1% ya wahojiwa hawakueleza chochote. Matokeo haya yanaonesha dhahiri kuwa mamlaka zinazosimamia utoaji wa

huduma ya usafiri jijini zinasimamiwa na sheria, kanuni na taratibu. Utafiti ulitaka kujua endapo kuna uzingativu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali na majibu yao yalikuwa kama ifuatavyo: asilimia 36.36% walikubali, asilimia 54.44% walikataa na asilimia 9.1% walisema hawajui chochote. Matokeo yanaonesha kuwa uwepo wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo peke yake, bila uadilifu na uaminifu wa watumishi waliopewa dhamana ya kukusanya mapato, Serikali hawezi kukusanya mapato kwa ufanisi.

4.1.1 Migongano ya Kisheria

Utafiti huu ulipitia sheria, kanuni na miongozo zinazoongoza Mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa mapato katika jiji la Dar es Salaam katika kituo cha mabasi yaendayo mikoani (Ubungo), maegesho ya magari na treni za abiria inayotoa huduma katika jiji. Utafiti umebaini uwepo wa migongano ya kisheria (conflicting laws) katika ukusanyaji wa mapato ya ushuru wa maegesho ya magari jijini ambapo sheria mbalimbali zinatoa mamlaka kwa wakusanyaji tofauti katika maeneo yale yale. Sheria zifuatazo zinatoa mamlaka ya kukusanya mapato:

(i) Kifungu cha 29 cha Sheria ya Barabara namba 13 ya mwaka 2007 inatoa mamlaka ya makusanyo ya fedha za maegesho/faini kwa Wakala wa Barabara TARURA na TANROADS;

(ii) Vifungu namba 29 na 31 vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 navyo vinatoa mamlaka kwa Halmashauri za Serikali za Mitaa/Manispaa/Majiji kukusanya mapato yakiwemo fedha za maegesho na stendi kwa kutumia mawakala;

(iii) Waraka namba 16 wa 2016 wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa Wakuu wa Mikoa (Tanzania Bara) kuhusu makusanyo ya mapato, matumizi ya mifumo ya kielektroniki (POS) katika ukusanyaji wa mapato na maeneo ambayo Serikali itatumia mawakala (CAB:110/156/01/26 wa 11 Julai 2016) ambapo aya ya 6(ii) inazitaka Halmashauri kukusanya mapato yatokanayo na ada za maegesho ya magari na ushuru wa stendi.

(iv) Barua ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye kumb. namba DA.347/371/01/13 ya 2018 kwenda kwa Makatibu Tawala wa Mikoa (Tanzania Bara) kuhusu makusanyo ya mapato yatokanayo na matumizi ya hifadhi za barabara zinazosimamiwa na TARURA. Aidha, barua hiyo inaeleza kuwa, kwa mujibu wa kifungu namba 3 cha Sheria ya Barabara Namba 13 ya 2007, TARURA ni Mamlaka ya Barabara na kwamba kifungu namba 29

kinaipa mamlaka TARURA kukusanya mapato kutokakana na ushuru wa maegesho ya magari ndani ya hifadhi ya barabara.

Sheria na miongozo hiyo inaruhusu ukusanyaji wa mapato/ushuru au ada za maegesho ya magari mijini kufanywa na zaidi ya Mamlaka moja katika maeneo hayo hayo na hivyo kusababisha migongano ya kiutendaji kati ya taasisi moja na nyingine. Mathalan, kwa mujibu wa Sheria ndogo ya Halmashauri ya Jiji ya Dar es Salaam ya GN 354 ya 2009, jiji linayo mamlaka ya kisheria ya kukusanya mapato katika maeneo yote ya Jiji. Wakati huo huo wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) inayo mamlaka kisheria ya kukusanya ushuru/ada ya maegesho ya magari katika maeneo ya hifadhi ya barabara za vijijini/mitaa ambazo hazipo katika hifadhi za barabara zinazosimamiwa na TANROADS (Trunk roads). Pia kwa upande wa TANROADS, utafiti umebaini kwamba taasisi hiyo imekuwa ikikusanya mapato yatokanayo na: (i) faini kutokana na ukiukwaji wa maegesho ya magari katika maeneo ya hifadhi ya barabara yasiyo ruhusiwa kisheria (wrong parking) na; (ii) upangishaji wa maeneo ya hifadhi ya barabara kwa watu binafsi kwa hifadhi za barabara inazosimamia na kuanzisha maeneo ya maegesho ya magari. Huu tayari ni mgongano wa kiutendaji (role conflict)

4.1.2 Matumizi ya Sheria Zilizofutwa

Utafiti umebaini kwamba Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inaendelea kutumia Sheria ndogo ya 2009 (Tangazo la Serikali Namba 354 la 23/10/2019) ya kukusanya mapato kwa Kituo Kikuu cha Stendi ya Mabasi ya Ubungo pamoja na maegesho ya magari lakini Sheria hiyo ilifutwa kwa kifungu namba 21 cha Sheria ndogo ya Tangazo la Serikali Namba 41 la 24/2/2017. Matumizi ya Sheria iliyofutwa inachangia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuendelea kupoteza mapato kutokana na baadhi ya ada kurekebishwa na kuongezewa kiwango tofauti na Sheria ndogo iliyofutwa ingawa bado inaendelea kutumika. Kwa mfano, Sheria ndogo ya 2009 iliyofutwa inaelekeza kuwa gharama za kulaza magari madogo ya mizigo katika kituo Kikuu cha Stendi ya mabasi Ubungo ni Tsh. 2000/- kwa siku wakati Sheria ndogo ya mwaka 2017 ni inaelekeza kuwa gharama za kulaza magari madogo ya mizigo (pick-ups) kwa siku ni Tsh.3000/- *(Rejea viambata namba E1 na E2).*

Utafiti umebaini kwamba licha ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, vifungu namba 6(1) na 16(1) kuzipa Mamlaka Serikali za Mitaa ya kukusanya kodi kupitia Sheria ndogo wanazoziandaa, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inatumia Sheria ndogo ya 2009 kukusanya mapato ya maegesho ya magari katika manispaa zote tano zinazounda Jiji la Dar es Salaam (Ubungo,

Temeke, Ilala, Kinondoni na Kigamboni). Kiuhalisia, Manispaa hizi zinazounda Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam nazo zina mamlaka kisheria ya kupanga vyanzo vya makusanyo ya mapato katika maeneo yao (*Rejea Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, vifungu namba 6(1) na 16 (1) na kiambatisho E3*).

4.1.3 Usimamizi Dhaifu wa Sheria

Utafiti umebaini kuwepo kwa usimamizi dhaifu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo unaochangiwa na migongano ya kisheria na uzembe wa baadhi ya watendaji kushindwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mikataba baina ya halmashauri na mawakala. Aidha, utafiti umebaini kuwa kuna watu binafsi ambao wameanzisha maegesho katika hifadhi za barabara zinazosimamiwa na TANROADS na hawatumii mashine za kielektroniki na kwa sababu hiyo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imekuwa haikusanyi mapato kwa madai kwamba maeneo husika ni mali ya TANROADS (Rejea kiambata E21).

4.2. Matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki katika Kukusanya Mapato ya Serikali

Utafiti ulitaka kujua endapo matumizi ya mifumo ya kielektroniki yamesaidia kurahisisha na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Katika kujibu swali hili, asilimia 85.7% ya wahojiwa walikubali kuwa matumizi ya mifumo ya kielektroniki yameongeza ukusanyaji wa mapato na asilimia 14.3% walisema hawajui kama matumizi ya mifumo ya kielektroniki imeongeza mapato ya Serikali.

4.2.1 Kituo cha Mabasi cha Ubungo

Wakati utafiti huu unafanyika, kwa upande wa stendi ya Ubungo, ilibainika kuwa mageti yote saba (7) na vyoo hakuna mashine hata moja ya ‘POS’. Watafiti walibaini kwamba wakusanya ada/ushuru wanatumia risiti za kielektroniki ambazo wamekuwa wakipewa na wahasibu/wasimamizi wa mashine za ‘POS’ na kwamba risiti hizo zinaposalia hurudishwa kwa mamlaka husika (*Rejea viambatisho E3 na E4).*

Mahojiano na Uongozi wa jiji pamoja na Meneja wa Stendi ya kituo cha mabasi cha Ubungo, yamebainisha kuwa risiti zote zinapaswa kutolewa kwa kupitia mfumo wa 'POS' na zinapaswa kutumika kwa tarehe husika tu na si vinginevyo (yaani siku moja tu). Hata hivyo, utafiti ulibaini kuwa idara ya uhasibu kwa kushirikiana na baadhi ya wakusanya ushuru/ada katika maeneo ya getini, chooni na sehemu nyingine za huduma, wamekuwa wakiuza tiketi za tarehe zilizopita kwa lengo la kuiibia Serikali na mauzo ya risiti hizo hufanyika mapema alfajiri. Huu ni mwanya wa upotevu wa mapato ya Serikali *(Rejea viambatisho E6, E7, na E8).*

Utafiti ulibaini kuwa watumishi wanaofanya kazi katika kituo cha mabasi cha Ubungo (waliopewa dhamana ya kukusanya mapato kwa niaba ya Serikali) hutumia tiketi ambazo wanapewa kutoka idara ya uhasibu ambazo hazioneshi muda ambao mteja amepata huduma. Aidha, utafiti umebaini kuwa baadhi ya watumishi wanaokusanya ushuru hupokea fedha pungufu kutoka kwa wateja, hawatoi risiti, huuza tiketi mara mbili na hubakiza risiti kwa lengo la kukusanyia ushuru ambao hautambuliwi na halmashauri ya jiji *(Rejea viambata E6, E7, na E8).* Huu ni mwanya wa upotevu wa mapato ya Serikali. Utafiti pia umethibitisha pasina shaka kuwa kutotumika kwa mfumo wa kieletroniki kukusanya mapato katika mageti yote saba na mfumo madhubuti wa kuratibu magari yanayolala ndani ya stendi kumesababisha upotevu wa mapato *(Rejea viambata E4 na E9).*

Utafiti huu ulitumia pia njia ya kushuhudia (observation) namna ukusanyaji wa mapato unavyofanyika kwa siku za tarehe 5-6 Novemba 2018, na kubaini yafuatayo:

(i) Kuna mauzo ya tiketi za siku zilizopita muda wake kwa wateja wanaoingia stendi na hivyo kuchangia kuhujumu mapato ya Serikali.Utafiti ulibaini kuwa uuzaji wa tiketi hizi hufanyika nyakati za asubuhi wakati wa msongamano wa wateja katika mageti *(Rejea viambata E6, E7, E8, E9 na E10)*

(ii) Kuna usimamizi mbaya wa makusanyo getini na kutokuwepo kwa mfumo wa kielektroniki wa kuhesabu mabasi yaliyolala stendi ili kulipa ada/ushuru stahiki kabla ya kuondoka stendi *(Rejea viambata E4,E9 na E10)* na*;*

(iii)Kwa siku ambazo TAKUKURU walisimamia ukusanyaji wa ushuru getini, mapato yaliongezeka katika kituo cha mabasi cha Ubungo kutoka Tsh.6,933,100 hadi

Tsh.7,321,800/- kwa siku, ikiwa ni ongezeko la Tsh. 388,700 kama inavyoonekana kwenye (*Rejea kiambatisho E11).* Hata hivyo, baada ya TAKUKURU kuondoka ukusanyaji wa mapato ulishuka tena hadi kufikia Tsh.6, 768,900 (ikiwa ni tofauti ya Tsh.552,900/- kwa siku) *(Rejea kiambata E11).*

(iv) Kwa upande wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kudhibiti uingiaji wa abiria ndani ya stendi, ilibainika kuwa kituo cha ubungo hakina mfumo mzuri wa kudhibiti watu wanaoingia na kutoka ndani ya kituo hicho ambako si tu huikosesha Serikali mapato bali pia inaweza kuhatarisha usalama wa abiria na mali zao *(Rejea kiambata E10).*

Aidha, kwa upande wa chanzo cha mapato katika eneo la Stendi Kuu ya Mabasi Ubungo ambalo makusanyo yake yanafanywa na Jiji la Dar es Salaam bila kutumia mawakala, takwimu zinaonesha limekuwa likikusanya kiwango cha chini tofauti na lengo iliyojiwekea. Mfano, matarajio ya makusanyo ya Jiji la Dar es Salaam kwa mwaka 2018/2019 katika kituo cha mabasi Ubungo ni Tsh. 2,399,855,805 (wastani wa Tsh.199, 987,983/-kwa mwezi). Hata hivyo, makusanyo ya juu kwa yaliyowasilishwa ni Tsh. 71,621,360 na ya chini ni Tsh. 24,514,650. (*Rejea viambata E14 na E15 ya Jedwali namba 2*). Matokeo haya yanaonesha kwamba halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam linapoteza mapato katika kituo cha Ubungo kutokana na kutozingatiwa kwa matumizi sahihi ya makusanyo ya fedha kwa njia ya kielektroniki (POS).

4.2.2 Maegesho ya Magari

Katika usimamizi za ukusanyaji wa mapato katika maegesho ya jiji la Dar es Salaam, utafiti ulitaka kujua endapo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imekuwa ikisimamia utekelezaji wa mikataba ya ukusanyaji na hatua inayochukua dhidi ya mawakala wanaokiuka makubaliano ya mikataba katika ukusanyaji wa mapato hususan katika suala la maegesho ya magari. Mikataba hii inatoa masharti kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kutoa mashine za ‘POS’ kwa mawakala kwa ajili ya ukusanyaji wa ushuru. Aidha, imebainika kwamba katika kipindi cha 2017/2018, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliingia mikataba na mawakala ‘M/S Excel Accountancy Services Limited’ kupitia mkataba (Lot 1) LGA/018/2017/2018/NCS/ 16, mnamo tarehe 1 /02/ 2018 na ‘M/S Chui Systems Limited’ kupitia mkataba (Lot 2) LGA/018/2017/2018/NCS/16 mnamo tarehe 26/01/2018. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa kwa kipindi cha kuanzia Februari 2018 na Novemba 2018 mawakala hao

wamekuwa wakikiuka makubaliano ya mkataba wa uwasilishaji wa mapato kwa mwezi na hakuna hatua iliyochukuliwa dhidi yao. Kwa mfano, 'M/S Excel Accountancy' kwa mujibu wa mkataba anatakiwa kuwasilisha kiasi cha fedha Tsh.716,050,000 kwa mwezi na M/S Chui Tsh.219,445,270.21 kwa mwezi. Hata hivyo, takwimu zinaonesha wakala 'M/S Excel Accountacy' ametekeleza makubaliano kama yalivyoainishwa kwenye mkataba kwa kipindi cha miezi miwili tu (yaani mwezi Mei na Julai, 2018); wakati 'M/S Chui Systems Limited' yeye hakuwahi kutekeleza masharti ya mkataba *(Rejea viambata E12, E13 na E14).*

Aidha, utafiti pia umebaini kuwepo kwa ukiukwaji wa matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato kwa kutumia 'POS' ambapo wakusanya ada/ushuru katika baadhi ya maeneo ya maegesho ya magari wamekuwa wakitumia risiti za kielektroniki wanazopewa na wasimamizi wao. Hata hivyo, utaratibu unaelekeza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inawajibika kutoa mashine za kielektroniki (POS) kwa mawakala wanaokusanya mapato kutoka vyanzo vya mapato yakiwemo cha maegesho ya magari. Vile vile kutozingatiwa kwa maelekezo ya matumizi ya mashine za POS ni chanzo cha upotevu wa mapato ya Serikali *(Rejea viambata E5, E12, E13 na E14).*

4.2.3 Treni ya Jiji

Licha ya Serikali kusisitiza matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika kukusanya mapato, bado uongozi wa 'TRL' unaosimamia uendeshaji wa treni ya jiji umeendelea kutumia risiti za kuandikwa kwa mikono badala ya risiti za kielekroniki *(Rejea viambata E16).* Utafiti ulitaka kupata uzoefu wa 'TAZARA' katika utumiaji wa mifumo ya Tehama na kuelezwa kuwa mifumo hiyo inaweza kuwa na tija endapo itasimamiwa vizuri na kuthibiti vitendo vya hujuma na udanganyifu vinavyofanywa na watendaji wasio waadilifu. Aidha, uongozi wa 'TRL', ulieleza kuwa mfumo wa kutumia risiti za kuchapa (manual systems) ni gharama kwa sababu ya kutumia wafanyakazi wengi na kuhitaji usimamizi wa karibu ili kudhibiti upotevu wa mapato. Hata hivyo, licha ya mafanikio wanayoendelea kupata, TAZARA wapo mbioni kutumia mashine za kielektroniki ili kuondoa udanganyifu unaoweza kutumiwa na baadhi ya wafanyakazi wasio waadilifu kutumia risiti za kuchapa kwa mkono na kuweza kuhujumu mapato yake *(Rea kiambata E16 na E17)*

Matokeo haya yanaonesha kuwa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato yanaweza kuongeza mapato endapo mianya yote ya rushwa itadhibitiwa pamoja na kuwasimamia kwa ukaribu watumishi waliopewa dhamana ya kukusanya mapato. Tafsiri ya matokeo haya ni kama ifuatavyo. *Mosi*: Halmashauri ya Jiji inapaswa kuweka mikakati madhubuti ya kuiziba mianya yote ya rushwa na kuongeza usimamizi wa watumishi. *Pili,* watumishi wote wa umma bila kujali nafasi zao watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa wachukuliwe hatua kwa mujibu wa Sheria. *Tatu,* Halmashauri iwekeze nguvu katika kutoa elimu ya rushwa kwa watumishi wake ikiwa ni pamoja na kuwataka kuzingatia maadili ya utumishi wa umma (Public Ethos) katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Sehemu inayofuata inahusu mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya kimkakati.

4.3 Mianya ya rushwa katika Ukusanyaji wa Mapato

Utafiti pia ulitaka kujua endapo kuna mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato hususan katika kituo cha mabasi cha Ubungo. Katika kujibu swali hili, majibu ya wahojiwa yalikuwa kama ifuatavyo: Asilimia 79 ya wahojiwa walikubali kuwa kuna mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato na asilimia 21 walisema hakuna mianya ya rushwa isipokuwa Serikali haijaweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi ikiwemo kuwapa motisha watumishi wanaohusika na kazi ya ukusanyaji wa ushuru. Utafiti ulibaini mianya ya rushwa katika maeneo nane (8) kama inavyoonekana hapa chini:

i. Uwepo wa utitiri wa Sheria na miongozo kinzani zinazosimamia ukusanyaji wa mapato katika eneo moja (conflicting laws). Sheria na miongozo hiyo ni pamoja na Sheria ndogo ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Tangazo la Serikali 41 la mwaka 2017 na Sheria ndogo ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Tangazo la Serikali namba 354 la 2009 ; Sheria ya Barabara namba 13 ya mwaka 2007 inayosimamiwa na TANROADS na TARURA; Vifungu namba 29 na 31 vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290; Barua ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye Kumb. Namba DA. 347/371/ 01/13 27 ya tarehe 27 Juni, 2018 na; Waraka namba 16 wa 2016 (CAB:110/156/01/26 wa 11 Julai 2016) wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa Wakuu wa Mikoa (Tanzania Bara) na; barua ya Mtendaji Mkuu wa TARURA kwenda kwa Waratibu wa TARURA Mikoa Tanzania Bara, barua yenye Kumb. Namba CAC.310/338/01/02 ya 29/6/2018 na; Barua ya Mratibu wa TARURA Mkoa wa Dar es Salaam kwenda Mkurugenzi wa Jiji kuhusu Mapato yatokanayo na hifadhi za

barabara zinazosimamiwa na TARURA (TRR/DRC/M.13/7/2 ya 4/7/18). Utafiti umebaini kuwa Sheria na miongozo husika zinaruhusu ukusanyaji wa ushuru wa maegesho ya magari kama vyanzo vya mapato katika Halmashauri za Serikali za Mitaa ikiwemo Jiji la Dar es Salaa na hivyo kusababisha migongano kati ya taasisi moja na nyingine *(Rejea vifungu namba 29 na 31 vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290, Sheria ya Barabara Namba 13 ya 2007 pamoja na viambatisho E1, E2, E5, E18, E19 na E20).*

ii. Ukiukwaji wa makusudi wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia ukusanyaji wa mapato unaofanywa na baadhi ya watendaji wasio waadilifu kwa lengo la kujinufaisha binafsi pasipo kuzingatia maslahi ya umma. Mfano, kitendo cha viongozi wa kituo cha mabasi cha Ubungo kugawa tiketi kwa wakusanya ushuru bila kuwapa mashine za 'POS', kitendo cha baadhi ya watumishi/wakusanya ushuru kuuza tiketi zilizopitwa na wakati (ambazo zimeisha matumizi yake), kitendo cha kutochukuliwa hatua stahiki kwa mawakala wanaoshindwa kutekeleza makubaliano ya uwasilishaji wa kiwango cha makusanyo ya fedha, kitendo cha watu binafsi walioanzisha maegesho ya magari baada ya kupangishwa na 'TANROADS' na kukata ushuru/ada bila kutumia mashine za 'POS' kwa pamoja vinathibitisha ukiukwaji wa makusudi wa sheria, kanuni na taratibu wenye lengo la kupoteza mapato ya Serikali (*Rejea viambatisho E4, E6, E7, E8, E9, E11, E12, E13 na E14).*

iii. Kuendelea kutumia sheria na kanuni zilizopitwa na wakati. Mathalani, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuendelea kukusanya ushuru ndani ya stendi ya Ubungo kwa kutumia Sheria Ndogo namba 354 ya mwaka 2009 (Toleo la 23/10/2009) badala ya kutumia Sheria Ndogo iliyotolewa kupitia Tangazo la Serikali (GN) Namba 41 la tarehe 24/02/2017 iliyofuta matumizi ya Sheria Ndogo ya mwaka 2009 *(Rejea viambatisho E1 na E2).*

iv. Kushindwa kusimamia vizuri (weak supervision) mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Utafiti umebaini kuna ukiukwaji wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato vikiwemo vitendo vya wizi na udanganyifu. Katika Kituo cha Ubungo ilibainika kwamba katika mageti yote 7 yaliyopo Stendi ya Ubungo hakukuwa na mashine yeyote ya kukusanyia mapato (POS) na pia mfumo wa kuhesabu magari yanayoingia, kulala na kutoka kituoni siyo wa kielektroniki na hivyo kuweka mazingira ya wizi na udanganyifu katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, Serikali imetoa mwongozo wa namna ya kuingia

mikataba baina ya halmashauri na mawakala pamoja na msisitizo wa matumizi ya mashine za kielektroniki (POS) katika kukusanya mapato *(Rejea kiambata E5).*

v. Tabia ya kuwasilisha mapato kiujumla bila kutoa mchanganuo unaoeleweka. Utafiti umebaini kuwa kuna vyanzo vingi vya ukusanyaji wa mapato katika stendi ya mabasi Ubungo lakini uwasilishaji wa taarifa za makusanyo ya mapato ya kila siku hauoneshi mchanganuo wa kila chanzo na kiasi kilichokusanywa na hivyo kutoa mwanya kwa baadhi ya watendaji kujihusisha na vitendo vya wizi na udanganyifu.

vi. Uholela na mpangilio mbaya wa biashara ndani ya stendi ya kituo cha mabasi cha ubungo. Utafiti umebaini hakuna utaratibu mzuri kuomba kufanya biashara ndani ya kituo cha mabasi, na hivyo kufanya kazi ya utambuzi wa wafanyabiashara kuwa ngumu.

vii. Uuzaji wa risiti zilizopitwa na wakati saa kumi na moja alfajiri wakati tayari risiti hizo hazitakiwi kutumika tena. Matumizi ya risiti zilizokwisha muda wake unaingiza hasara Serikalini kwa kuwa risiti hizo huwa tayari zinahesabika kuwa zimerudishwa kwa mamlaka husika kwa lengo la kuweka mlinganisho (reconciliation) katika vitabu vya mahesabu ya mwajiri *(Rejea viambata E6, E7 na E8).*

viii. Kumekuwepo na vitisho toka kwa baadhi ya watumishi wa vyombo vya dola (extortion) dhidi ya viongozi wanaosimamia kituo cha mabasi cha Ubungo kwa kuwataka watoe ‘chochote’ vinginevyo watawachukulia hatua au kuwashughulikia! Vilevile, utafiti umebaini kuwa baadhi ya watumishi wa Jeshi la Polisi wamekuwa wakiomba kupewa huduma za chakula kwa gharama za kituo cha mabasi cha Ubungo.

5.0 Muhtasari wa Matokeo

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kubaini endapo kuna vitendo vya rushwa katika ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya kimkakati katika jiji la Dar es Salaam. Ili kufikia lengo hili, utafiti huu uliongozwa na madhumuni mahsusi manne ambayo ni: (i) kubaini endapo kuna usimamizi duni wa sheria, kanuni na taratibu na miongozo katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kwenye miradi ya usafirishaji (ii) kubaini endapo matumizi ya mifumo ya kielektroni yamesaidia kuongeza mapato ya Serikali na (iii) kubaini endapo kuna mianya ya rushwa katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato. *Mosi*, utafiti umethibitisha uwepo wa usimamizi duni wa sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia ukusanyaji wa mapato katika miradi ya usafiri jiji unaochangiwa na migongano ya kisheria na

kitaasisi na matokeo yake ni Serikali kukosa mapato au kukusanya kiasi kidogo cha mapato chini ya matarajio yake. *Pili,* utafiti umethibitisha kuwa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato hayajaweza kuongeza mapato ya Serikali kwa sababu ya matumizi madogo, usimamizi duni na tabia ya baadhi ya watendaji kuihujumu mifumo hiyo ili isindwe kufanya kazi kwa ufanisi. *Tatu,* utafiti umethibitisha pasina shaka uwepo wa mianya ya rushwa ipatayo [kumi na moja] inayosababisha Serikali kukosa mapato yanayotokana na utekelezaji wa miradi ya usafiri katika jiji la Dar-es-salaam.

6.0 Mchango wa Utafiti katika Utungaji Sera na Utendaji

Matokeo ya utafiti huu yanatoa mchango mkubwa katika utungaji wa sera, sheria, kanuni na taratibu na namna zinavyopaswa kutekelezwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Jambo kubwa la kujifunza katika utafiti huu ni kwamba kuwa na mfumo mzuri wa ki-sera na kisheria ni jambo moja na kuwa na uwezo wa kusisimamia na kuzitekeleza sera na sheria ni jambo lingine. *Pili*, utitiri wa sera na Sheria sio mbadala wa uwajibikaji, uadilifu na weledi wa watendaji wa ngazi mbalimbali katika utumishi wa umma. *Tatu*, matokeo haya yanaonesha umuhimu wa Serikali kuendelea kutoa elimu ya rushwa katika maeneo ya kazi. *Nne,* matokeo haya yanamaanisha kuwa taasisi za umma zinapaswa kufanya kazi kwa kushirikiana na si kwa kushindana. Ni vema utungaji wa sera/sheria ukazingatia malengo ya kila taasisi, mipaka yake kisheria na kiutendaji ili kuepusha migongano isiyo ya lazima. *Tano,* matokeo haya yanaonesha umuhimu wa Serikali kuendelea kuwekeza zaidi katika kazi za utafiti na uchambuzi wa mifumo ya utoaji huduma ili kuyabaini maeneo yenye udhaifu na kupendekeza mikakati ya kuimarisha mifumo hiyo.

MAPENDEKEZO

LENGO	MATOKEO	PENDEKEZO	MHUSIKA
Kubaini endapo ukusanyaji wa mapato unazingatia na kusimamia sheria, kanuni, taratibu na miongozo hususan katika sekta ya usafiri wa umma jijini Dar-es-salaam	Utafiti umebaini kuwa kuna usimamizi dhaifu wa ukusanyaji wa mapato katika kituo cha mabasi cha ubungo na mfumo wa kukusanya ushuru wa maegesho ya magari katika Jiji la Dar es Salaam unaochangiwa na mgongano ya kisheria na kitaasisi.	➢ Kufanya uchambuzi wa kina wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo zinazokinzana kwa lengo la kuainisha vifungu vinavyoingiliana/kugongana na kuzipatanisha (harmonize) kwa minajili ya kuondoa migongano ya kisheria kati ya taasisi moja ya umma na nyingine (Lack of coherence). ➢ Mipaka ya kiutendaji kati ya taasisi moja na nyingine iwekwe wazi kwa minajili ya kuondoa misuguano ya ki-taasisi isiyo kuwa ya lazima (institutional clashes).	Tume ya Kurekebisha Sheria (Tanzania Law Reforms Commission)
Kubaini endapo matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato yamesaidia kuongeza mapato	➢ Ukiukwaji wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato na hivyo kusababisha upotevu wa mapato stahiki ya Serikali. ➢ Vitendo vya hujuma na udanganyifu vinavyofanywa na baadhi ya watumishi wasio waadilifu kwa lengo la kupata manufaa binafsi kwa tiketi watu wanaoingia ndani ya kituo cha mabasi cha ubungo tiketi zilizokwishatumika, kukaidi kwa makusudi kutumia mashine za ‘POS’ kwa lengo la kuibia Serikali na mawakala kutowasilisha makusanyo halisi kama mikataba	➢ Kuimarisha usimamizi wa watumishi waliopewa dhamana ya kukusanya mapato kwa kutumia mifumo ya kielektroniki hususan ‘POS’ na kuwachukulia hatua watumishi wasio waadilifu wanaohujumu mifumo ya kukusanya mapato kwa makusudi ili kujinufaisha. ➢ Kuanzisha uchunguzi wa ukukwaji wa matumizi ya mashine za kielektroniki (POS) katika kukusanya mapato katika vyanzo vya maegesho ya magari na kituo cha mabasi Ubungo	Katibu Mkuu - TAMISEMI; Mkurugenzi Mkuu - TAKUKURU

	inavyotaka..	➢ Maafisa uchunguzi wa TAKUKURU wapewe 'Mafunzo Maalum' ya namna mashine za 'POS' zinavyofanya kazi ili kuweza kubaini na kudhibiti hujuma.	
Kubaini endapo kuna mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya kimkakati	Ukiukwaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayofanywa na watumishi wasio waadilifu kwa lengo kujipatia manufaa binafsi	➢ Elimu ya Mapambano dhidi ya rushwa iendelee kutolewa. ➢ Wanaokakiuka sheria, kanuni na taratibu, na kujihusisha na vitendo vya rushwa hatua kali zichukuliwe mara moja dhidi yao bila woga wala upendeleo.	TAMISEMI Halmashauri ya Jiji la Dar-es-Salaam, TAKUKURU
	Matumizi ya sheria ndogo (by-laws) zilizopitwa na wakati.	Uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam utekeleze Sheria Ndogo ya 2017 badala ya 2009 iliyofutwa.	Halmashauri ya Jiji la Dar-es-Salaam.
	Usimamizi dhaifu wa mifumo ya kielektroniki hususan 'POS'	➢ Uongozi wa Halmashauri ya jiji l;a Dar es-salaam uimarishe usimamizi kwa kuhakikisha kila wakala anawasilisha makusanyo yote kwa wakati kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo; na kuchukua hatua kali kwa watakaokiuka ikiwemo kuwafikisha mahakamani kwa kosa la wizi. ➢ Ukusanyaji wa mapato uzingatie taratibu na miongozo ya Serikali kuhusu 'POS'. ➢ 'TRL' wazingatie matumizi ya risiti za kielektroniki na kuacha risiti za kuandikwa kwa	Halmashauri ya jiji la Dar-es-salaam TRL TRL

		mkono	
	Uwasilishaji wa mapato kiujumla kwa lengo la kuficha kiasi halisi cha fedha kilichokusanywa na kila chanzo cha mapato	Kila mtumishi au wakala anapaswa kuwasilisha kiasi halisi kilichokusanywa kutoka katika kila chanzo bila kificho kwa ajili ya kurahisisha uwekaji wa kumbukumbu utunzaji wa mahesabu na uwajibikaji.	Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.
	Mpangilio mbaya wa biashara ndani ya kituo cha mabasi cha Ubungo na hivyo kufanya usimamizi na ukusanyaji wa ushuru kuwa mgumu	Uongozi wa stendi ya kituo cha mabasi cha Ubungo uhakikishe unawatambua wafanyabiashara wote wanaofanya shughuli zao ndani ya kituo cha mabasi cha ubungo na kuimarisha usimamizi. Hii itarahisisha zoezi la ukusanyaji wa ushuru unaotokana na biashara hizo kuliko ilivyo sasa.	Halmashauri ya jiji la Dare-es-Salaam
	Udanganyifu na uuzaji wa tiketi zilizopitwa na wakati kwa lengo la kujipatia manufaa binafsi unaofanywa na baadhi ya watumishi wasio waadilifu	Uongozi wa halmashauri ya jiji la Dare-es-Salaam uimarishe usimamizi wa watumishi wanaokaa magetini na watakaojihusisha na vitendo vya udanganyifu wachukuliwe hatua za kisheria haraka iwezekanavyo.	Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

7.0 Hitimisho

Serikali zote duniani hupimwa kwa namna zinavyoweza kuwahudumia wananchi wake kwa kutoa huduma bora za kijamii. Kushindwa kukusanya kodi ni moja ya dalili zinazoonesha kushamiri kwa rushwa katika Serikali yoyote. Nadharia za kiuchumi zinaonesha kuwa hakuna mbadala wa kodi na kwamba wananchi wanapaswa kulipa kodi kwa ustawi na maendeleo ya nchi zao. Kwa mantiki hiyo, vitendo vyote vya rushwa, ubadhirifu, wizi katika mifumo ya ukusanyaji wa kodi ni lazima vidhibitiwe. Mifumo ya utoaji huduma inapaswa kufanyiwa tathmini za mara kwa mara kwa lengo la kubainisha maeneo yenye udhaifu na kupendekeza hatua muafaka za kuiimarisha. Watendaji waliopewa dhamani ya kukusanya kodi wanapaswa kufanya kazi zao kwa uadilifu. Elimu ya rushwa kwa watumishi wa umma inapaswa kuwa endelevu ili kuwakumbusha wajibu wao wa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu. Rushwa na utawala bora ni maadui. Ili kupata mafanikio, kila mwananchi anapaswa kujiepusha na vitendo vyote vya kuomba na kupokea rushwa, na badala yake waunge mkono jitihada za Serikali za kupambana na rushwa kwa kutoa taarifa sahihi kwa TAKUKURU.

MAREJEO

Barua Kumb. Namba CAC.310/338/01/02 ya 29 Juni 2018 ya Mtendaji Mkuu wa TARURA kwenda kwa Waratibu wa TARURA Mikoa: Makusanyo ya Mapato na Matumizi ya Hifadhi za Barabara zinazosimamiwa na TARULA

Barua ya Katibu Mkuu OR-TAMISEMI kwenda kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, DA.347/371/01/13 ya 27/6/2018 –Makusanyo ya Mapato yatokanayo na Hifadhi za Barabara zinazosimamiwa na TARURA

Barua ya Mratibu wa TARURA Mkoa wa Dar es Salaam kwenda kwa Mkurugenzi wa Jiji kuhusu Mapato yatokanayo na hifadhi ya Barabara zinazosimamiwa na TARURA

Mkataba wa makusanyo ya maegesho ya magari baina ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na M/S Excel Accountancy Services Limited, LGA/018/2017/2018/NCS/16, Lot 1 (Januari 2018)

Mkataba wa makusanyo ya maegesho ya magari baina ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na M/S Chui Systems Limited, LGA/018/2017/2018/NCS/16, Lot 2 (Januari 2018)

Sheria ndogo ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam GN 41 ya 24/2/2017, Udhibiti wa vyombo vya usafiri na uboreshaji wa mapato

Sheria ndogo ya Jiji la Dar es Salaam GN namba 354 la 23/10/2009, makusanyo ya mapato Kituo cha Mabasi Ubungo

Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290

Sheria ya wakala wa barabara Tanzania namba 13 ya 2007

Taarifa ya Makisio na Mapato halisi ya makusanyo ya mapato (Ada za mabasi Ubungo na uegeshaji wa magari), Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuanzia mwaka 2015/2016, 2016/2017 na 2017/2018

Taarifa ya makusanyo ya pesa ya huduma ya usafiri wa treni ya TAZARA

Waraka Namba 16 wa mwaka 2016 wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI Kuhusu Halmashauri mwongozo wa makusanyo ya mapato kwa kutumia Mawakala, Matumizi yam ashine za POS na maeneo ya vyanzo vya mapato ambavyo Halmashauri hawatakiwi kutumia Mawakala, CAB: 110/156/01/26 wa 11 Juni 2018

VIAMBATISHO

E1-Kiambata namba 1: Sheria ndogo ya Jiji la Dar es Salaam GN namba 354 la 23/10/2009, makusanyo ya mapato Kituo cha Mabasi Ubungo

E2-Kiambata namba 2: Sheria ndogo ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam GN 41 ya 24/2/2017, Udhibiti wa vyombo vya usafiri na uboreshaji wa mapato

E3-Kiambata namba 3: Idadi ya Risiti za Kielektroniki zilizouzwa na kusalia katika kituo cha mabasi Ubungo

E4-Kiambata namba 4: Wakusanya ushuru wa getini wakiwa hawana mashine za POS

-E5-Kiambata namba 5: Waraka Namba 16 wa mwaka 2016 wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI Kuhusu Halmashauri mwongozo wa makusanyo ya mapato kwa kutumia Mawakala, Matumizi yam ashine za POS na maeneo ya vyanzo vya mapato ambavyo Halmashauri hawatakiwi kutumia Mawakala, CAB: 110/156/01/26 wa 11 Juni 2018

E6-Kiambata namba 6: Sehemu za Risiti za kuingia mageti ya Stendi ya mabasi Ubungo za Tsh. 300/-zinazosomeka tarehe 6/11/2018 wakati zilizonunuliwa na maafisa wa TAKUKURU tarehe 07/11/2018

E7-Kiambata namba 7: Moja ya Risiti ya huduma ya Choo ya Tsh.200/-inayosomeka tarehe 5/11/2018 ambayo ilinunuliwa na Afisa wa TAKUKURU tarehe 6/11/2018 majira ya saa 10: 32 alfajiri

E8-Kiambata namba 8: Sehemu **ya r**isiti za Tsh.300/-kuingia katika mageti ya kituo cha mabasi Ubungo zikionesha tarehe 5/11/2018 lakini ziliuzwa kwa maafisa wa TAKUKURU tarehe 6/11/2018

E9-Kiambata namba 9: Uratibu mbaya wa mabasi yanayolala Ubungo ambapo mfumo wa kuhesabu magari ili kulipa ada stahiki ni kwa kuhesabu kawaida (manual counting) badala ya mfumo wa kielektroniki wa kutambua gari linaloingia na kutoka kituoni

E10-Kiambata namba 10: Usimamizi mbaya wa makusanyo katika mageti ya Stendi ya Mabasi Ubungo.

E11-Kiambata namba 11: Makusanyo ya fedha katika mageti ya kituo cha mabasi Ubungo baada ya ofisi ya TAKUKURU kufanya zoezi la udhibiti tarehe 5-6/11/2018

E12-Kiambata namba 12: Mkataba wa makusanyo ya maegesho ya magari baina ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na M/S Excel Accountancy Services Limited

E13-Kiambata namba 13: Mkataba wa makusanyo ya maegesho ya magari baina ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na M/S Chui Systems Limited

E14-Kiambata namba 14: Makusanyo ya mapato kwa kutumia mawakala kwa chanzo cha maegesho ya magari na makusanyo ya mapato yanayofanywa na Jiji lenyewe katika Kituo cha Mabasi cha Ubungo

E15-Kiambata namba 15: Taarifa ya Makisio na Mapato halisi (Ada za mabasi Ubungo na uegeshaji wa magari) kuanzia mwaka 2015/2016, 2016/2017 na 2017/2018

E16-Kiambata namba 16: Sehemu ya risiti za mkono zinazotumika katika usafiri wa Treni ya TAZARA na TRC

E17-Kiambata namba 17: Taarifa ya makusanyo ya mapato TAZARA

E18-Kiambata namba 18: Barua ya Katibu Mkuu OR-TAMISEMI kwenda kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, DA.347/371/01/13 ya 27/6/2018 –Makusanyo ya Mapato yatokanayo na Hifadhi za Barabara zinazosimamiwa na TARURA

E19-Kiambata namba 19: Barua Kumb. Namba CAC.310/338/01/02 ya 29 Juni 2018 ya Mtendaji Mkuu wa TARURA kwenda kwa Waratibu wa TARURA Mikoa: Makusanyo ya Mapato na Matumizi ya Hifadhi za Barabara zinazosimamiwa na TARULA

E20 Kiambata namba 20: Barua ya Mratibu wa TARURA Mkoa wa Dar es Salaam kwenda kwa Mkurugenzi wa Jiji kuhusu Mapato yatokanayo na hifadhi ya Barabara zinazosimamiwa na TARURA

E21-Kiambata namba 21: Moja ya sehemu ya maegesho ya magari ya mtu binafsi baada ya kupangishwa eneo na TANROADS.